

**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKARI ZA MITAA(TAMISEMI)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

Tel:+255(0)758046931

Tel:+255(0)624106683

SHULE YA SEKONDARI BUDALABUJIGA,  
S.L.P 234,  
BARIADI,  
SIMIYU.

Kumb.Na. BUSS/F.1/2020/012

Tarehe: 15/12/2020.

JINA LA MWANAFUNZI.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS) JANUARI 2020.**

Mkuu wa shule ya sekondari Budalabujiga anayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kuijunga na masomo ya Elimu ya sekondari katika shule ya sekondari Budalabujiga.Masomo haya yatakuwa ya muda wa miaka isiyopungua minne (4) na yatatolewa bila malipo.Masomo yataanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kufika shulenii kuanzia tarehe 11/01/2021 na tarehe ya mwisho ya kuripoti shulenii ni 20/01/2020.**AMBAPO BAADA YA TAREHE HIYO KUPITA NA IKIWA HUJARI POTI SHULENI HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.**

**1. MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ya Sekondari Budalabujiga ipo Kata ya Budalabujiga,Tarafa ya Kanadi,Wilaya ya Itilima Mkoo wa Simiyu.Shule ipo kilomita 10 kutoka makao makuu ya Wilaya ya Itilima kando ya barabara ielekeayo Bariadi.Shule hii ni ya serikali na niya kutwa na ni shule ya mchanganyiko (wavulana na wasichana).

**2. MASUALA MUHIMU WAKATI WA KURIPOTI SHULENI**

**2.1 SARE YA SHULE**

Utatakiwa kushona sare ya shule yaani nguo maridadi,nadhifu na yenyeye kuonyesha haiba nzuri kama ifuatvyo:-

**2.1.1 WAVULANA**

- Suruali moja kitambaa cha suti nyeusi yenyeye “U-turn”
- Suruali moja ya kitambaa cha suti Bluu-bahari yenyeye “U-turn”
- Shati mbili au zaidi mikono mifupi nyeupe
- Tai nyeusi moja mpya
- Tai bluu bahari moja mpya
- Soksi nyeusi zisizo na alama yeyote
- Viatu vyeusi vya ngozi vinavyo funika miguu

**2.1.2 WASICHANA**

- Sketi moja kitambaa cha suti nyeusi ya kushona yenyeye marinda box ya saizi ya inch 2 na sio mitumba, Sketi ifike kwenye kiwiko cha miguu na isiwe na mpasuo.
- Sketi moja kitambaa cha suti bluu bahari ya kushona yenyeye marinda box ya saizi ya inch 2 na sio mitumba, Sketi ifike kwenye kiwiko cha miguu na isiwe na mpasuo
- Shati mbili au zaidi mikono mifupi nyeupe.
- Skafu nyeupe moja mpya